**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA KISARAWE**
**(Barua zote ziandikwe kwa Mkurugenzi Mtendaji (W)**

***Unapojibu tafadhali taja:***
**Kumb.Na.KDC/F.20/24/VOL.V/13** **16 Julai,2024**

**TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI YA MUDA ZA WASIMAMIZI WA UKUSANYAJI MAPATO YA HALMASHAURI KWENYE VIZUIA**

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kisarawe anayo furaha kuwatangazia wananchi wa Kisarawe wenye sifa na uwezo wa kufanya kazi ya usimamia ukusanyaji mapato kwenye vizuia mbalimbali.

Nafasi hizo kama zifuatazo:

1. **Mkusanya Mapato – Nafasi 42**

**1.1 <u>Sifa za Mwombaji:-</u>**

- Awe na elimu ya kidato cha nne na kuendelea.
- Awe amepitia mafunzo ya angalau cheti katika masuala ya serikali za Mitaa, Uhasibu, Sheria au Maendeleo ya Jamii.
- Mwenye uwezo wa kufanya kazi ya ukusanyaji mapato kituo chochote Wilayani.
- Mwadilifu na mwenye kujituma
- Awe na umri kuanzia miaka 21 hadi 40 na awe raia wa Tanzania.
- Awe anajua kutumia simu janja.

**1.2 <u>Majukumu ya Kazi</u>**

i. Kukusanya mapato na kulipa kwa kutumia kifaa kiitwacho POS
ii. Kuhakikisha makusanyo yote yanapelekwa benki kwa wakati, ndani ya saa 24 .
iii. Kutumia mfumo mbadala/ wa nje pale mtandao unapokosekana na kuingiza kwenye mfumo husika pale mtandao unapokuwepo.

CamScanner

**Masharti ya jumla**

1. Waombaji wote waambatishe nakala ya Cheti cha kuzaliwa.
2. Waombaji waambatishe maelezo binafsi (CV) yenye anuani na namba za simu za kuaminika na wawe na wadhamini mawili wenye namba za NIDA, picha, namba za simu na mmojawapo wa wadhamini ni mtumishi wa umma.
3. Maombi yaambatishwe na picha moja (Passport size ya hivi karibuni na iandikwe jina kwa nyuma).
4. Maombi yaambatishwe na nakala za Vyeti vya Taaluma/Shule na Vyeti vya kuhitimu mafunzo ya Vyuo.
5. Waombaji wote waambatishe nakala ya Kitambulisho cha Taifa (NIDA) – kwa ambao hawana vitambulisho, namba za NIDA ziandikwe kwenye maelezo (CV).
6. Maombi yote yawasilishwe kupitia Ofisi ya Masijala kwa kutumia anauni ifuatavyo:-

*Mkurugenzi Mtendaji,*
*Halmashauri ya Wilaya ya Kisarawe,*
*S.L.P 28001,*
***KISARAWE.***

***MWISHO WA KUPOKEA MAOMBI NI TAREHE 31/07/2024 SAA 9.00 ALASIRI.***

***NB: Tangazo hili pia linapatikana katika Tovuti ya Halmashauri ambayo ni www.kisarawe.go.tz, mbao za matangazo Ofisi za Kata.***

*Imetolewa na;*

Beatrice R. Dominic
**MKURUGENZI MTENDAJI,**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA KISARAWE.**

MKURUGENZI MTENDAJI (W) S.L.P 28001, KISARAWE